**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMAKUHUSU UTARATIBU WA UTOAJI WA CHANJO YA HOMA YA MANJANO KWA WATANZANIA NA WAGENI WANAOSAFIRI NJE YA NCHI

**DODOMA: 18 Oktoba, 2025**

Wizara ya Afya inapenda kuukumbusha umma wa Watanzania kuhusu utaratibu wa kupata **chanjo ya homa ya manjano** ambayo ni muhimu kuchanjwa wanapopata safari ya nje ya nchi, ili kuwa na kinga dhidi ya ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Muongozo wa Taifa wa huduma ya Chanjo ya Homa ya Manjano uliohuishwa na Wizara ya Afya mwezi Novemba 2023, pamoja na miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO), mtu anayepata chanjo hiyo huhesabika kuwa na kinga ya kudumu, hivyo haihitajiki kuchanja tena na anapaswa kupewa Cheti maalum cha Kimataifa cha Chanjo (Yellow Card).

Wasafiri wote wanakumbushwa kubeba vyeti vyao halali vya chanjo ya homa ya manjano ambayo inatolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya mipakani, Hospitali ya Mnazi Mmoja, bandarini, uwanja wa ndege wa kimataifa na Hospitali ya Taifa Muhimbili pindi wanaposafiri nje ya nchi, ili kuepuka usumbufu wanapofika mipakani, bandarini na kwenye viwanja vya ndege.

Wizara ya Afya inatoa wito kwa wananchi wote kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya kuhusu chanjo za ulinzi, kuhakikisha wanapata chanjo hizi kwa wakati sahihi angalau siku 10 kabla ya safari na kuhifadhi vyeti hivyo kwa matumizi ya safiri.

Vilevile, Wizara ya Afya inasisitiza kuwa hakuna ulazima wa kuchanjwa tena ikiwa mtu tayari amechanjwa na ana uthibitisho wa kuwa na cheti halali kilichotolewa na Wizara ya Afya katika vituo vyetu rasmi.

Imetolewa na:

**Roida Andusamile**
**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**